

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOZA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOZA**

**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
**S.L.P 5429,**  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MKUU WA MKOZA WA DAR ES SALAAM MHE. PAUL MAKONDA APOKEA MWENGE WA UHURU.**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul C. Makonda amekabidhiwa Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mhe. Godfrey Zambi mara baada ya kumaliza shughuli za uzinduzi na ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo Mkoani Lindi.

Mwenge huu wa Uhuru utakuwepo Mkoani Dar es Salaam kwa siku tano kuanzia leo tarehe **27/05/2017** hadi tarehe **31/05/2017** ambapo pamoja na mambo mengine **zaidi ya miradi ipatayo arobaini (40)** ya kimaendeleo yenye thamani ya **Tshs 244,392,530,334/= itapitiwa**, ambapo miradi mikubwa **kumi na mbili (12) itazinduliwa**, vilevile miradi mitano **(5) itawekewa mawe ya msingi**, pia **miradi miwili (2) itafunguliwa rasmi** na **miradi kumi na moja (11) itatembelewa** katika Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika hotuba yake kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Makonda amewahamasisha wananchi wake kudumisha Umoja na Mshikamano, Mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria na Maambukizi ya VVU/UKIMWI na kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Madawa ya kulevya.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOZA WA DAR ES SALAAM**

27/05/2017